# NOVENA KWA MTAKATIFU RITA WA KASHIA



Mtakatifu Rita Mwombezi wa Mambo Yasiyowezekana

**Mwogozo wa Sala kwa Siku zote Tisa za Novena na Siku Tatu za Shukrani**

katoliki.ackyshine.com

# NOVENA SIKU YA KWANZA

**Kwa jina la Baba,na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Ee Mtakatifu Rita mfanya miujiza,uniangalie kwa macho yako yenye huruma,mimi ninaye teseka na kutoa machozi. Uone moyo wangu unaotoka damu umezungukwa na miiba. Yaonr macho yangu, ee Mtakatifu Rita,kuwa hayatoki machozi tena kwani machozi mengi yamenitoka!

Nimechoka na kukata tamaa. Nimechoka pia kusali. Je, nikate tamaa katika misukosuko hii ya maisha yangu? Uje! Ee Mtakatifu Rita, njoo hima unisaidie. Je, wakristo hawakuiti Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana na mwombezi wa waliokata tamaa? Basi dhihirisha ukuu wa jina hilo, kwa kunijalia toka kwa Mungu yote ninayokuomba *(hapa omba hitaji lako unalotaka kumwomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita).*

Kila mtu anasifia utakatifu wako. Kila mtu anasimulia maajabu na miujiza Mungu anayotenda kwa njia yako. Je,mimi tu nitakataliwa na kukatishwa tamaa kwa vile hujanisikia? Hapana. Uniombee kwa Bwana Yesu ili anionee huruma na kunisaidia katika masumbuko na mahangaiko yangu. Kwa maombezi yako, Ee Mtakatifu Rita,niweze kupokea kile ambacho moyo wangu unatamani sana.

**Baba yetu ×3 Salamu Maria ×3 na Atukuzwe Baba ×3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita:- homa,madonda na tauni,viini vya maradhi mbalimbali,mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu , viziwi, bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako:- radi,tetemeko la ardhi na moto havina nguvu. Kwa utakatifu wako mitego yote,hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako . Kashia hutukusa jina lako. Unawasaidia vipofu , viziwi, bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu na kwa Mwanae ziwe sifa,utukufu na heshima,sifa kwa karne zote za pendo la milele. Unawasaidia vipofu , viziwi, bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

**Kiongozi :** Umemtia alama Ee Bwana,mtumishi wako Rita.

**Wote:** Kwa mhuri wa upendo na mateso.

**<u>TUOMBE</u>**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema,hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako,ili tupate tuzo ulilotuahidia kwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala,daima na milele. Amina.

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA PILI

**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina**

Ewe mfanya miujiza Mtakatifu Rita wa Kashia. Naona njia ya maisha yako imejaa majaribu na miiba mingi inayochoma, ambayo nahofia imepasua moyo wako vipande vipande. Ee Rita uliye kweli shahidi wa maumivu makali. Uliyeonja tone kwa tone, hadi ukamaliza kikombe chote cha maumivu makali. Nafikiria juu ya moyo wako uliochoka kabisa. Ninakugeukia na kumwomba Mungu kwa maombezi yako *<u>(hapa omba hitaji lako unalotaka kumwomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita).</u>*

Wewe unajua maana ya moyo unaovuja damu. Unajua pia kifodini cha roho. Umeumizwa sana na kuteseka sana. Kwa njia ya mateso hayo nakuomba unisaidie katika mahangaiko yangu. Jesi kweli kwamba wakati huu mgumu, Bwana wetu Yesu

ametuandalia njia ya kujipatia neema; kupitia miujiza ambayo binadamu wanaweza kukuomba kwa matumaini na kwa maombezi yako wakafanikiwa?

Ee Mtakatifu mpenzi, iangalie roho iliyopondeka inayolia na kuhuzunika mbele yako. Ninakutumainia, Ee Mtakatifu Rita. Niombee kwa Yesu mbinguni ili nipate kupokea yote ninayomwomba Mungu kwa maombezi yako yenye nguvu.

**Baba Baba Yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita:- homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako:- radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu. Kwa utakatifu wako mitego yote, hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako. Kashia hutukuza jina lako. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu, na kwa Mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima, sifa kwa karne zote za pendo la milele. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

**Kiongozi:** Umemtia alama, Ee Bwana, mtumishi wako Rita.

**Wote:** Kwa mhuri wa upendo na mateso.

**<u>TUOMBE:</u>**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidi kwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele. Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA TATU

**Kwa jina la Baba,na la Mwana,na la Roho Mtakatifu.Amina**

Natazama huku na huko bila ya kupata mahali pa mapumziko,huku macho yangu yakiwa yametiwa uvuli kwa uchungu. Matarajio yoyote ya dunia hii hayauchangamshi moyo wangu unaosononeka kwa uchungu,najiona nimepotea kabisa. Lakini wewe kipenzi Mtakatifu Ritha,unaye ng'ara kama nyota inayoangaza kwa mwanga usio kifani katika nguvu na nguzo za kanisa katoliki,natambua wewe unaimulika njia yangu yenye giza na unaupa shime moyo wangu unaoomboleza kwa uchungu. Ninakuamini,kwa hamu nangojea,kupata kile nikiombacho *<u>(hapa omba hitaji lako unalotaka kumwomba Mungi kupitia Mtakatifu Ritha)</u>*

Nifikshie ombi langu kwa Yesu wa msalaba.Nakumbuka kipindi kile kigumu kwako wakati moyo wako ulipopata majaribu,kwa utii ulipokubali kufunga ndoa na mtu ambaye alikutesa hata kutishia maisha yako. Hata hivyo ulimpenda sana na alipofariki uliomboleza kifo chake kwa huzuni kuu. Kwa sadaka yako ya kishujaa,uliyomtolea Mungu wana wako,ukiomba wasinajisiwe kwa dhambi.Uniombee kwa Mungu.Hicho ni kifo dinicha moyo wako.

Kupitia mateso ambayo Bwana Yesu kristo aliruhusu yakupate ili utakaswe katika majonzi yako,kwa njia ya majiribu mengi yaliyokupata na sadaka nyingi ulizotoa,uniombee ili nijaliwe kupewa ombi langu ninalongojea kwa hamu.

**Baba Yetu(3),salamu maria(3)na atukuzwe Baba(3)**

Kwa njia ya Mtakatifu Ritha ;homa,madonda na tauni ,viini vya maradhi mbalimbali,mapepo na ghadhabu vitoweke umewasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana wafu wanarudishiwa uhai

kwa maombezi yako;radi,tetemeko la ardhina moto havina nguvu.kwa utakatifu wako mitego yote,hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana.Watu wengi wanaimba sifa zako.Kashia hutukuza jina lako unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

Kwa Mungu Mtakatifu,na kwa mwanae ziwe sifa,utukufu na heshima,sifa kwa karne zote za pendo la milele unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

**Kiongozi :** umemtia alama,ee Bwana mtumishi wako Rita

**Wote:** kwa mhuri wa upendo na mateso

**TUOMBE**

Ee Mungu uliyekubali kutawadha Mtakatifu Ritja kwa neema,hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso.Tunakuomba kupitia maombezi yake neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya metso yako,ili tupate tuzo uliotuhadia kwa wapole na wanaoteseka.Unayeishi na kutawala daima na milele Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA NNE

**Kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina**

Ee Mtakatifu wa yale yaliyoshindikana,na wakili wa waliokata tamaa.Hizi ni sifa safi zenye kujaa tumaini kwa roho zenye kujaribiwa na uchungu.Kwako wewe Mtakatifu Rita wa kashia,ambaye wakati tunapojikuta pweke katika maisha yetu,tunapozungukwa na huzuni na kifo,wewe watujia kama mtunza bustani kutoka mbinguni kutuletea ndani ya mioyo yetu iliyokauka tumaini na maji yaliyo hai.

Ee tumaini la moyo wangu ulikauka kutokana na msongo mkubwa wa huzuni;uzito wa maafa umenielemea,mashaka yananiogofya na sijui nielekee wapi kutafuta msaada ninaohitaji.kwako wewe Rita mwema,ninakuamini sana na kukutegemea;nakujia nikiwa na uhakika utanisikiliza. Kwa nguvu ya maombezi yako

mbele ya kiti cha enzi cha Mungu,natumaini kusikilizwa katika ombi langu *(hapa omba hitaji lako unalotaka kumwomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita)*

Jionyeshe tena kuwa u mwenye nguvu na huruma.Nithibitishie pia kuwa ni kweli kama wafuasi wako wanavyokukili kuwa Mtakatifu wa yale yaliyoshindikana, na wakili wa waliokata tamaa.

**Baba Yetu(3), Salamu Maria(3) na Atukuzwe Baba(3).**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita; homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako;radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu.kwa utakatifu wako mitego yote,hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako.Kashia hutukuza jina lako. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu,na kwa Mwanae ziwe sifa,utukufu na heshima,sifa kwa karne zote za pendo la milele. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

**Kiongozi :** Umemtia alama, Ee Bwana,mtumishi wako

**Rita.** Wote :kwa mhuri wa upendo na mateso.

**TUOMBE:**

Ee Mungu,uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema,hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso.Tunakuomba kupitia maombezi yake,neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako,ili tupate tuzo ulilotuahidia kwa wapole na wananoteseka.Unaeishi na kutawala,daima n milele.Amina.

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA TANO

**Kwa jina la baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Ewe mchumba mpendwa wa Yesu, Mtakatifu Rita wa Kashia; nakuja kwako tena. Nipo miguuni pako. Navutwa na wema wako kwa Roho zenye kutaabika na kusumbuka. Unaona moyo wangu ulivyo pondwapondwa kwa magumu ya dunia hii. Sipati tena tabasamu la thanani, Roho yangu imevamiwa na mashaka mabaya. Imani imetetereka na mshituko wa kukata tamaa kama msituko wa kifo unapiga miayo miguuni pangu. Nielekeze, Ee Mtakatifu mpendwa nifanye nini katika mazingira haya ya kutisha? Nishauri nimwendee nani katika hali ya hatari katika maisha yangu.

Kama kweli wewe ni Mtakatifu wa hali zote za kukatisha tamaa, njoo unisaidie kwani najisikia ninepotea. Nakuja kwako wewe ambaye kila mara wawahurumia wanaoteseka. Nakuja kwako unisaidie. Je, hutanionea huruma kutokana na hali yangu? Mtakatifu Rita najua u mwema sana. Najua hivyo , ndio maana najiweka mikononi mwako kwa moyo wangu wote ili unijibu kwa njia ya Yesu, lile ombi langu ambalo kwa imani naliomba *( hapa omba  hitaji lako unalotaka kunwomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita )*

**Baba yetu (3), Salamu Maria (3), na atukuzwe baba(3).**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita: homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete:watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako:- radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu. Kwa utakatifu wako mitego yote, hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispania wanakutangaza kuwa mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba fadhili zako. Kashia hutukuza jina lako. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu  na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu mtakatifu, na kwa mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima,sifa za karne zote za pendo la milele: Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

**Kiongozi :** umemtia alama, Ee bwana , mtumishi wako Rita.

**Wote :** kwa muhuri wa upendo ma mateso.

**TUOMBE:**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha mtakatifu Rita kwa Neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, Neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidi kwa wapole na wanao teseka. Unayeishi na kutawala , daima na milele .Amina.

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA SITA

**Kwajina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Nafahamu kwa sababu ya dhambi zangu sala zangu zimefunikwa na wingu zisiweze kufika katika kiti chako cha enzi. Dhambi zangu ni sababuya adhabu zangu kubwa. Sina ujasiri wa kuelekeza sauti yangu kwa YESU. Kwakua mara nyingi sikuthamini huruma yake. Na sasa naiona nguvu yake kuu na ya haki. Mkono wake wa haki umenielekea. Natambua kwamba sistahili baraka za msamaha wake kwani nimegubikwa na huzuni kubwa. Pasipo na matumaini nayalilia madhambi yangu.

Niambie Mtakatifu Ritha, Je, niendelee kukata tamaa? Hapana. Bwana wetu YESU KRISTO amekuteua kuwa mtetezi wake mwenye nguvu ili uniombee kwa Yesu wangu aliye juu,msamaha kwa makosa yangu makubwa na nia safi ya kumtotendea dhambi tena.

Kwa uamuzi huu thabiti,wa midomo yamgu na moyo wangu,nakuelekea wew. Eee Mtakatifu mtenda miujiza,uniombee kwa Bwana Yesu fadhila ambazo nazihitaji sasa *( hapa omba hitaji lako unalotaka kumuomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita)* Katika muda huu wa uchovu mkubwa,huzuni na kuachwa pweke, Ee Rita, neno lako kwa Yesu litafungua huruma na msamaha wake. Sema neno na Yesu atakusikia.

**Baba Yetu 3, Salamu Maria 3 na Atukuzwe Baba 3.**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita ~ homa, madonda na tauni,viini vya maradhi mbalimbali mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

Kwa maombezi yako : radi tetemeko la ardhi na moto havina nguvu. Kwa utukufu wako mitego yote ,hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako. Kashia hutukuza jia lako. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete:watoto wanaomba sanana wafu wanarudishiwa uhai

**Kiongozi :** Umemtia alama ,Ee Bwana mtumishi wako Rita.

**Wote :** Kwa mhuri wa upendo na mateso.

**TUOMBE :**

Ee Mungu, uliyekubali kutawadha Rita kwa neema,hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake ,neemaza kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako,ili tupate tuzo uliotuahidia kwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele. Amina.

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA SABA

**Kwa jina LA Baba, nala Mwana, nala Roho Mtakatifu . AMINA.**

Ee mpedwa Rita, ambaye maisha yako yalikuwa yahuzuni. Nielekezee uso wako wa huruma mimi mwenye maumivu makali. Naomba sala zangu, uchovu wangu na kuchechemea kwangu viufikie moyo wako mpole ili uweze kufunguliwa kwangu. Huruma yako ambayo wakati wote uliionesha kwa Jiran, maneno ya aman na faraja, na ushauri Mtakatifu uliowapa watu wote vinivute kukuelekea wewe uliye katika mbingu na unakoishi na kuwa mwombezi wa watu wote waliokata tamaa.

Mbele ya miujiza yako mikuu, kifo kinarudi nyuma, vipofu wanapokea nuru, viwete wanasimama, waliopooza wanaponyeshwa na ulemavu wote wa roho na mwili unaondoka kabisa. Je! Nipo peke yangunjsiyefarijiwa na maombezi yako? Sitaamini wala siwezi kuamin hivyo. Nam naamini kwa dhati usimamizi wako na maombezi yako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Ninamatumaini makubwa kuwa nitapata amani, moyoni wang, utulivwana fadhila ninazoomba nitajaliwa, *[ hapa omba hitaji lako unalotaka kumwomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita]*

**Baba yetu×3, Salam Maria×3, na Atukuzwe Baba×3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita~ homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

Kwa maombezi yako~ radio, tetemeko LA ardhi na moto havina nguvu, kwa utakatifu wako mitego yote, hatari na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete ; watoto wanaomba sana na watu unawarudishia uhai.

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo wa mambo yaliyoshindikana, watu wengi wanaimba sifa zako Kashia hutukuza jina lako; Unawasaidia vipofu viwete bubu na viziwi, watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu, nakwa mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima, sifa kwa karne zote za Pendo la milele. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete , watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

**Kiongozi:** Umemtia alama Ee Bwana, mtumishi wako Rita.

**Wote:** Kwa muhuri wa upendo na mateso.

**Tuombe:**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohon mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yako, neema za kusamehee adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidia kuwa Wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele . Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA NANE

**Kwa jina la Baba,na la Mwana, na la Roho Mt. Amina**

Ewe kielelezo kitakatifu cha Msalaba Mtukufu, ninapokuona ukiwa umesujudu mbele ya miguu mitakatifu ya Bwana,ninapotafakari paji la uso wako lililojeruhiwa kwa mwiba uliotoka ktk taji la miiba la Yesu Kristo, mchumbawako mpendwa, imani yangu kwako inachanua kwa namna ya ajabu. Wewe ni mtumishi mteule wa Mungu. Mungu amekuzawadia alama ya ufalme wake akakutakatifuza na kukufanya uwe mali yake kabisa .

Hivyo sikukosea nilivyoweka imani yangu yote kwako,na nilipojiweka kabisa chini ya ulinzi wako wenye huruma nyingi. Na sasa ni wakati mzuri wa kunisaidia, ukiyajua mahitaji na misaada ninayoomba kutoka kwako. Naamini sala hii kwako wewe mama mpenz sana haitapotea bure.

Wew uliye mfanya miujiza, mfadhili wa mambo ya mbinguni, unayetegemewa na wanadamu wote. Ninakuomba na kukusihi kwa mastahili ya pendo lako kwa Yesu Kristo Mwokozi wetu, uniombee ili nijaliwe haya niombayo *( hapa omba hitaji lako*

*<u>unalotaka kumwomba Mungu kupitia Mtakatifu Ritha)</u>* Mungu hakukatalii wew kitu chochote; kwa maombezi yako,miujiza hufanywa,neema na fadhila maalumu hupatikana. Hivyo, kwa moyo wangu wote na matumaini ya dhati,ninasubiri nikitegemea kupata haya niliyoomba kwa Bwana Mungu.

**Baba Yetu 3, Salamu Maria 3 na Akukuzwe Baba 3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita; homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako: radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu, kwa utakatifu wako mitego yote, hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete; watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispani wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako. Kashia hutukuza jina lako ; Unawasaidia vipofu viwete bubu na viziwi, watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu, na kwa Mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima, sifa kwa karne zote za Pendo la milele. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete , watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

**Kiongozi :** Umemtia alama Ee Bwana, mtumishi wako Ritha.
**Wote:** Kwa muhuri wa upendo na mateso.
**<u>Tuombe;</u>**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidia kuwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele . Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# NOVENA SIKU YA TISA

**Kwajina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Nina kuja mbele yako, Ee Mtakatifu Rita, siku hii ya mwisho ya Novena hii Takatifu. Ninayasikia mapigo ya moyo katika kipindi hiki kigumu cha maisha yangu yaliyogawanyika. Ninaamini kwamba ombi langu litatimizwa na Bwana kupitia maombezi yako Matakatifu. Lakini ikiwa haiwezekani,ninapaza sauti nikiomba kwanguvu huruma na faraja yako. Usiniache niondoke bila kupata faraja yako.

Ee Mtakatifu Rita ,ninaomba unifariji kwa mastahili ya mateso uliyoyapata hapa duniani na katika upweke wako wa sala. Unifariji kwa mastahili ya ukarimu uliokua nao kwa wenye shida unisikilize kwa kwa mastahili ya upendo wako mkuu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, na kwa mama yake Bikira Maria Mtakatifu asiye na doa. Kwa mastahili ya ule mwiba Mtakatifu aliokujalia Bwana wetu Yesu Kristo,unisaidie na unifadhili mimi.

Hiki ndicho kilio changu cha mwisho kwako wewe mama uliye Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana na mwombezi wa waliokata tamaa. Ninakuomba ujidhihirishe katika mwanga wako halisi, ili Mungu anijalie haya ninayo yaomba. *(hapa omba hitaji lako unalotaka kumuomba Mungu kupitia Mtakatifu Rita)*

Kwa msaada wako ninadhamiria kuachana na mwenendo wangu potofu, ili niwe muenezaji wa nguvu za Mungu na uzuri wa mambo ya Mbinguni. Ninaahidi pia mahali pako pa upweke, Ee Mtakatifu wa sala,huko Kashia,na au kwenye sanamu yako: ili niweze kuungana nawe katika kuabudu na kushukuru kwa fadhila za Mbinguni nilizozipata kwa maombezi yako kutoka kwa Mwokozi wetu Azizi Yesu Kristo.

**Baba Yetu 3, Salamu Maria 3, Atukuzwe 3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita : homa, madonda na tauni,viini vya maradhi mbalimbali na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai .

Kwa maombezi yako: radi,tetemeko la ardhi na moto havina nguvu. Kwa utakatifu wako mitego yote,hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete :watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

Hispania wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mabo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako.Kashia hutukuza jina lako. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

Kwa Mungu Mtakatifu na kwa mwanae ziwe sifa,utukufu na heshima,sifa kwa karne zote za pendo la milele. Unawasaidia vipofu,viziwi,bubu na viwete : watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai

**Kiongozi :** Umemtia alama Ee Bwana, mtumishi wako Rita.

**Wote :** Kwa mhuri wa upendo na mateso.

**<u>Tuombe:</u>**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema,hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako ili tupate tuzo ulilotuahidia kwa wapole na wanaoteseka . Unayeishi na kutawala, daima na milele. Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# SHUKRANI KWA HESHIMA YA MAOMBEZI YA MTAKATIFU RITHA WA KASHIA

## SIKU YA KUMI (Siku ya kwanza ya shukrani)

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.  Amina.**

Baba wa milele! Ambaye huruma yako haina mwisho, na wema wako ni wa milele. Niangalie nikikusujudia kwa unyenyekevu mbele ya kiti chacko cha Enzi kitukufu. Nainua kutoka chini ya moyo wangu utenzi wa kukushukuru kwa upendo ulionijalia kupitia mtumishi wako Rita wa Kashia. Natambua eeh Mungu wangu kuwa sistahili kupata fadhila ulizonikirimia na kwa kutokujali mapungufu yangu bali umenisikiliza sala yangu kwa maombezi ya mtakatifu Rita wa Kashia.

Ee mtakatifu Rita mfanya miujiza maarufu wa kanisa katoliki; kwako ninakutolea shukrani zangu za dhati. Kinywa changu hakina maneno ya kutosha ya kueleza jinsi ninavyojisikia moyoni mwangu. Ee mtakatifu mpenzi;ni kweli kwamba wote wanaotumainia maombezi yako hawakatishwi tamaa. Nijaze daima neema ambayo naweza kupata kupitia huruma ya Mungu na unijalie ulinzi wako katika maisha na kifo.

**Baba Yetu3,  Salamu Maria3 na Akukuzwe Baba3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita; homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako: radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu, kwa utakatifu wako mitego yote, hatari  kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete ; watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispani wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako. Kashia hutukuza jina lako. Unawasaidia vipofu viwete bubu na viziwi, watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu, na kwa Mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima, sifa kwa karne zote za Pendo la milele. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete , watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

**Kiongozi :** Umemtia alama Ee Bwana, mtumishi wako Ritha.

**Wote:** Kwa muhuri wa upendo na mateso.

**TUOMBE;**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidia kuwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele . Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# SIKU YA KUMI NA MOJA (Siku ya Pili ya Shukrani)

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Ee Moyo mpendelevu wa Yesu, ulio daima na utajiri na ukarimu wa huruma isiyo na mwisho. Na ambaye ulimwambia nabii kuwa sikifurahii kifo cha mtu mwovu bali ageuke na kuishi, uniangalie katika unyonge wangu.

Nakushukuru wewe Kwa moyo wangu wote na Kwa neema za pekee ulizonijalia kupitia fadhila za mtumishi wako mteule, Mtakatifu Rita wa Kashia. Je? Nitakurudishia nini, Ee Bwana, kwa upendo ulionijaloa? Ee Mungu wangu sitaacha daima kukushukuru Wewe ambaye daima umekua mwema kwa wote wanaokudharau.

Nawe mpenzi Mtakatifu Rita, nikulipeje fadhila ulizonijalia? Moyo wangu umejaa furaha isiyo kifani. Nitakushukuru bila mwisho. Ee mtakatifu mwema, uliye

karibu na Bwana wetu; nipelekee Shukrani zangu kwake na kwako na kuwa daima nitaichukia dhambi ili niendelee kufaidi huruma yake na maongozi yake ya mbinguni.

**Baba Yetu3, Salamu Maria3 na Akukuzwe Baba3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita; homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako: radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu, kwa utakatifu wako mitego yote, hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka . Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete ; watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispani wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako. Kashia hutukuza jina lako ; Unawasaidia vipofu viwete bubu na viziwi, watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu, na kwa Mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima, sifa kwa karne zote za Pendo la milele. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete , watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

**Kiongozi :** Umemtia alama Ee Bwana, mtumishi wako Ritha.

**Wote:** Kwa muhuri wa upendo na mateso.

**Tuombe;**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidia kuwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele . Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (ipo mwisho wa sala zote)**

# SIKU YA KUMI NA MBILI (Siku ya tatu ya shukrani)

**Kwa jina la Baba,na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina**

Ee Mungu wangu mpendwa, ambaye huwaachi wanye kukutumaini na wenye kukuamini wapate mateso, bali kwa upendo wasikiliza sala zao. Toka kilindini mwa moyo wangu nakutolea shukurani zangu za daima kwa fadhila ulizonijalia kwa maombezi ya mtumishi wako uliyemchagia, Mt Rita. Pokea ,Ee Bwana Yesu, shukurani zangu za dhati, zitokazo kama harufu nzuri ya sadaka. Pokea kupitia mikono ya Mt Rita. Ee Yesu mpenzi, nisaidie ili daima niwe macho kupokea ukarimu wako, wema wako na huruma yako

Pamoja nawe,Ee Mtakatifu mtenda miujiza , ambaye jina lako linatukuzwa kwa furaha kubwa dumiani kote na ambaye maombezi yako huleta miujiza; pokea shukurani zangu toka kilindini mwa moyo wangu. Ningetamani kila mtu akujue; watu wote wakupende. Kwani watu wote wangetambua nguvu zako za mbinguni

Ee nyota angavu ya Shirika la Mt Augustino; katika kutoa shukurani kwa mema niliyopata kwa fadhila nyingi, nitaeneza kwa watu wote ibada yako;nikiwaambia watu kuwa wewe kweli ni Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana, mwombezi wa walio kata tamaa, mwombezi wa wote waliopoteza matumaini ya dunia hii

**Baba Yetu3, Salamu Maria3 na Akukuzwe Baba3**

Kwa njia ya Mtakatifu Rita; homa, madonda na tauni, viini vya maradhi mbalimbali, mapepo na ghadhabu vitoweke. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete: watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa maombezi yako: radi, tetemeko la ardhi na moto havina nguvu, kwa utakatifu wako mitego yote, hatari kubwa na vitisho vyote hutoweka. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete ; watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Hispani wanakutangaza kuwa Mtakatifu wa mambo yaliyoshindikana. Watu wengi wanaimba sifa zako. Kashia hutukuza jina lako ; Unawasaidia vipofu viwete bubu na viziwi, watoto wanaomba sana na wafu wanarudishiwa uhai.

Kwa Mungu Mtakatifu, na kwa Mwanae ziwe sifa, utukufu na heshima, sifa kwa karne zote za Pendo la milele. Unawasaidia vipofu, viziwi, bubu na viwete , watoto wanaomba sana na wafu unawarudishia uhai.

**Kiongozi :** Umemtia alama Ee Bwana, mtumishi wako Ritha.

**Wote:** Kwa muhuri wa upendo na mateso.

**<u>Tuombe;</u>**

Ee Mungu, uliyekubali kumtawadha Mtakatifu Rita kwa neema, hata akakubali kuwapenda adui zake hadi akapata rohoni mwake na katika paji la uso alama za upendo na mateso. Tunakuomba kupitia maombezi yake, neema za kusamehe adui zetu na kutafakari maumivu ya mateso yako, ili tupate tuzo ulilotuahidia kuwa wapole na wanaoteseka. Unayeishi na kutawala, daima na milele . Amina

**Litania Kwa Mtakatifu Rita wa Kashia……. (Ipo mwisho wa sala zote)**

# LITANIA KWA MT RITA WA KASHIA

Bwana Utuhurukie, Kristo Utuhurumie, Bwana Utuhurumie,

**Kiitikio "Utuhurumie"**

Baba wa Mbinguni, Mungu,

Mwana Mkombozi wa Dunia,Mungu, Roho Mtakatifu, Mungu,

Utatu Mtakatifu, Mungu Mmoja,

Maria Imakulata Mama wa Mungu…………………….. **Kiitikio "Utuombee"**

Maria, Mama mfariji wa wanaoteseka Maria, Malkia wa Watakatifu wote Maria,

Mwombezi mpenzi wa Mt Rita…………………….. **Kiitikio "Utuombee"**

Mt Rita, Zawadi toka Mbinguni …………………….. **Kiitikio "Utuombee"**

Mt Rita, Mwombezi wetu mwenye nguvu: Mt Rita, uliyejaliwa Utukufu:

Mt Rita, mstaajabiwa tangu utoto wako: Mt Rita, mpenda upweke:

Mt Rita, Kielelezo cha usafi wa moyo: Mt Rita, kielelezo cha upole wote:

Mt Rita, kielelezo cha mke mwema:

Mt Rita, kielelezo bora cha mama mtaratibu: Mt Rita, kielelezo cha msamaha wa kweli: Mt Rita, kielelezo hai cha kujikatalia:

Mt Rita, kioo cha maisha ya kitawa: Mt Rita, kioo cha utii;

Mt Rita, mvumilivu wa kustajabiwa; Mt Rita, shujaa wa kujitoa sadaka;

Mt Rita, shahidi katika kufanya toba; Mt Rita, mjane mtakatifu;

Mt Rita, mkarimu kwa masikini;

Mt Rita, mkereketwa wa kuitikia wito mtakatifu; Mt Rita, aliyeingizwa utawani kimuujiza;

Mt Rita, harufu nzuri ya manemane; Mt Rita, bustani ya kila fadhila;

Mt Rita, mpendezwa na Yesu Msulubiwa;

Mt Rita, uliyechomwa na mwiba kwenye paji la uso; Mt Rita, binti mpendevu wa Bikira Maria;

Mt Rita, mwenye kiu ya upendo wa Kimungu; Mt Rita, uliyevikwa utukufu;

Mt Rita, lulu ya mbinguni;

Mt Rita, utukufu wa shirika la Mt Augustino; Mt Rita, tunu ya thamani ya Umbria;

Mt Rita, mwenye nguvu za utakatifu;

Mt Rita, msamaha wa wanaopata mahangaiko; Mt Rita, mfariji wa wanaoteseka;

Mt Rita, nanga ya wokovu;

Mt Rita, mwombezi wa wagonjwa;

Mt Rita, mwombezi wa mambo yaliyoshindikana; Mt Rita, kimbilio la walio hatarini;

Mt Rita, msaada wenye nguvu kwa wote; Mt Rita, mastaajabio ya ulimwengu;

Mt Rita, uliyepokewa mbinguni kwa furaha;

Mwanakondoo wa Mungu uondoae dhambi za dunia, "Utusamehe Bwana"

Mwanakondoo wa Mungu uondoae dhambi za dunia, "Utusikilize Bwana"

Mwanakondoo wa Mungu uondoae dhambi za dunia "Utuhurumie"

**Kiongozi:** Umemtia alama Ee Bwana mtumishi wako Rita

**Wote:** Kwa mhuli wa upendo na mateso

**Tuombe:**

Ee Mungu , ambaye katika wema wako wa daima, umependa kusikiliza maombezi ya mtumishi wako Rita. Utujalie kupitia maombezi yake, yale ambayo yameshindikana kwa nguvu za kibinadamu. Utuhurumie sisi tunaoteseka, uwasaidie wote wasiokuamini wajue kuwa wewe ni tuzo la wanyenyekevu, mfariji wa wote wenye hofu, na nguvu ya wanyonge. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina

***Kila baada ya kusali novena ya siku, tunasali litania hii kwa siku zote 12***

**Copyright © All Rights Reserved, Ackyshine**

***Tembelea katoliki.ackyshine.com Kupata majarida mengine***